

"Kesheni basi kwa maana hamjui siku wala saa." Mt 25:13

Mnamo siku ya Jumanne Tarehe 2 Machi, 2021, saa 11:30 alfajiri Mwenyezi Mungu alimwita kwake Mtumishi wake Baba Abate wetu

Mh. Pd. Placidus (Peter) Mtunguja OSB

Baba Abate Placidus alizaliwa tar 21. 02. 1963, kwa wazazi Paul Yohana na Mama Fabiana Seleman Gao; katika Parokia ya Sakarani jimbo la Tanga. Alikuwa ni mtoto wa tano kati ya wanane wa wazazi hawa. Alibatizwa tarehe 23. 03. 1963 na kupewa jina la Peter. Alipata Sakramenti za mwanzo za Ubatizo, Komunio ya kwanza na kipaimara kama kawaida.

Baada ya kumaliza shule ya msingi huko Kwekitui mwaka 1983, Peter alivutiwa kujiunga na Shirika la Watawa wa Kibenediktini baada ya kuona mfano mzuri wa Paroko wake na Mmisionari maarufu Pd. Bukhard Scheider, OSB. Hivyo mwaka 1984 alijiunga na Seminari ndogo ya Wakapuchini huko Maua Moshi, kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Sita na kuhitimu mwaka 1990.

Mwaka huo 1990 alikuja Ndanda kuanza kujifunza na kuisha maisha ya kitawa. Mwaka 1991 hadi 1994 alisoma masomo ya Falsafa huko Arusha, Seminari Kuu ya Shirika la Roho Mtakatifu (Holy Ghost Fathers). Mwaka 1994 aliingia katika hatua ya Unovisi na kupewa jina la Placidus maana yake *'Mpole'* Mwaka 1996 alifunga Nadhiri za Kwanza za Kitawa na mwaka 2000 alifunga Nadhiri za Daima katika Abasia ya Ndanda.

Mwaka 1991 hadi 1994 Abate Placidus alisoma masomo ya Falsafa (Philosophy) huko Njiro Arusha na kujipatia Shahada kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Urbaniana Roma. Mwaka 1996 hadi 2000 alisoma Masomo ya Tauhidi (Theology) huko Seminari ya Salvatorian Morogoro. Siku hizi kinaitwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan. Alifanya tena mtihani kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Urbaniana na kupata Shahada ya Tauhidi. Licha ya masomo hayo, Abate Placidus amehudhuria Semina mbali mbali za Malezi na Uongozi huko Roma miaka tofauti tofauti.

Baba Abate Placidus, katika maisha yake alikuwa na haiba kubwa ya Uongozi. Katika ngazi zote za malezi, Baba Placidus alikuwa Kiongozi wa wenzake. Hivyo, haikuchukua muda kwa walezi wake kugundua Karama hiyo na kumwendeleza ili awe Mlezi wa baadae. Mwaka 1999-2000 alipokuwa katika mwaka wa Kichungaji, ili kujiandaa kwa Daraja la Ushemasi na Upadre, Baba Placidus aliwekwa kuwa Mlezi msaidizi katika Nyumba ya Malezi. Mara baada ya Upadrisho alipangwa mara katika Nyumba ya Malezi kusaidia na kuwafundisha wanaokuja kuanza maisha ya Kitawa. Na mwaka 2002 hadi 2010, alikuwa Mlezi wa Wanovisi.

Mwaka 2015, tulifanya uchaguzi wa Abate katika Abasia yetu ya Ndanda. Baba Placidus alichaguliwa kuwa Abate wa Tano wa Abasia ya Ndanda. Pia alikuwa Abate wa Kwanza Mwafrika, baada ya kipindi kirefu cha Uongozi wa Watawa Wamisionari toka Ulaya. Hii ilitokana na tunu za uongozi zilizoonekana ndani yake.

Katika uongozi wake, Baba Abate Placidus alikuwa kweli ***'Baba'*** kama Mtk. Benedikto anavyoelekeza katika Kanuni yake, kuwa Abate awe Baba kwa mfano wa maisha yake na mafundisho yake.
Baba Abate Placidus alikuwa kiunganishi kizuri cha Uongozi wa Watawa Wamisonari na sisi Watawa wenyeji. Aliweza kutuunganisha bila kutugawanisha. Aliweze kuendeleza misingi ile ile iliyowekwa na wazee wetu, Kiroho, Kiutawala na hata Kiuchumi; kwa kifupi, aliendeleza vema kauli mbiu ya Kibenediktini ya SALA na KAZI (Ora eti labora).

Baba Abate Placidus, hakuwa na historia ya kuumwa au kuwa na magonjwa ya kudumu. Muda wote alionekana mwenye afya njema na mchangafu. Ni kawaida yake mwanzo wa mwaka hutembelea ndugu na nyumba zetu, na alifanya hivyo. Pia alishiriki matukio mbalimbali ya Kikanisa na Kitaifa. Baba Abate Placidus, alirejea Ndanda tar 15 February 2021. Na Jumatano ya majivu aliongoza Misa na hata kutoa Mafundisho (Conference) kwa Jumuia. Hata hivyo alijisikia mchovu labda kutokana na urefu wa safari aliyofanya.

Mnamo tarehe 17/02/2021 Abate Plasidus alifika Hospitalini Ndanda, akisumbuliwa na maumivu ya kichwa na uchovu; vipimo vya awali havikuonesha tatizo hivyo akatibiwa kama mgonjwa wa nje na kuruhusiwa kwenda nyumbani, akitumia dawa na kushauriwa kupumzika. Tarehe 23/02/2021 Abate Plasidus alirudi hospitalini baada ya kumaliza dawa alizopewa kwa siku tano akiwa bado hajapata nafuu, kichwa bado kilikuwa kikimsumbua, pia mwili kukosa nguvu na pia awamu hii alikuwa akisumbuliwa na kikohozi. Tarehe 25/02/2021 hali ya mgonjwa alianza kudhoofu zaidi, ambapo iliwalazimu madaktari kumwekea *'oxygen'* kwa ajili ya kumsaidia kupumua huku akiendelea na dawa.

Tarehe 25-28/02/2021 hali ya mgonjwa ilikuwa inabadili badili. Mara anapata nafuu kubwa na mara anadhoofu tena. Jopo la madaktari lilitaka kumsafirisha kwenda Hospitali nyingine, lakini haikuwezekana kutokaba na mabadiliko ya mara kwa mara ya hali yake. Walitegemea apate nafuu kidogo kisha kumsafirisha. Hata hivyo, madaktari wa hapa Ndanda na wale washauri nje ya Ndanda, walijiridhisha kuwa yupo kwenye tiba sahihi.

Tarehe 01/03/2021 ilimbidi wampelekea chumba cha uangalizi maalum ICU. Saa 10:45 alfajiri, hali ya mgojwa ilibadilika na kiwango cha oxygen kwenye damu kilishuka gafla, hivyo madaktari bingwa pamoja na wataalamu wa dawa ya usingizi wakakubaliana kumwekea mashine ya kumsaidia kupumua. Mgojwa alifanikiwa kuwekwa kwenye mashine lakini hali haikuimarika na moyo ulisimama. Walijitahidi kumfanyia “Cardio Pulmonary Resuscitation” (CPR) lakini ilishindikana na saa 11:30 Alfajiri Baba Abt. Placidus akafariki dunia.

Tunashukuru Madakari, Madaktari bingwa na Wauguzi wa Hospital ya Ndanda kwa juhudi zao kubwa kutaka kuokoa maisha ya mpendwa wetu. Pia tunashukuru Madaktari washauri wa Hospitali moja huko Dar es Salaam, ambao walikuwa karibu sana katika matibabu yake. Tunashukuru ndugu watawa na wote waliomhudumia kwa upendo wa hali ya juu. Tunashukuru pia ndugu zake wa damu akiwepo kaka yake Pd. Anton Mtunguja, toka Tanga. waliofika kumuuguza. Mungu awabariki sana.

Baba Abate Placidus aliacha wosia wa pekee kwa wale waliokuwa karibu naye dakika za mwisho za maisha yake. Alisema; nakukuu: “*Muwe waaminifu” na pia alisema “Serikali isifanye mchezo mchezo na ugonjwa huu,”* bila kufafanua Zaidi.

Baba Abate Placidus amefariki akiwa na umri wa miaka 58 ya kuzaliwa, akikaribia miaka 25 ya utawa *(hapo tar 29. 06. 2021)* na alikaribia miaka 20 ya Upadre *(hapo 14. 07. 2021). Na miaka 6 ya uabate.*

“Bwana ametoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana na lihimidiwe.”

Imetolewa na Br. Yohanes Mango OSB, Prior.
Na Watawa wa Abasia ya Ndanda
Tarehe 9 Marchi 2021.